Arusha, Tanzania
Tovuti: www.african-court.org
Simu: +255-27-970-430

**MUHTASARI WA HUKUMU**

# MATOKE MWITA NA MASERO MKAMI DHIDI YA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**MAOMBI NA. 007/2016**

**HUKUMU KUHUSU**
**UZINGATIAJI WA SHERIA NA FIDIA**

**TAREHE 13 JUNI 2023**

**UAMUZI WA MAHAKAMA YA AFRIKA YA HAKI ZA BINADAMU NA WATU**

**Arusha, tarehe 13 Juni 2023:** Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu (Mahakama), leo, imetoa Hukumu katika kesi ya *Matoke Mwita na Masero Mkami dhidi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.*

Matoke Mwita na Masero Mkami ni raia wa Tanzania ambao, wakati wa kuwasilisha Maombi haya, walikuwa wamefungwa katika Gereza Kuu la Butimba, Mkoa wa Mwanza, wakitumikia kifungo cha maisha baada ya kukutwa na hatia ya makosa ya ubakaji wa kikundi na unyang'anyi wa kutumia nguvu. Maombi yalifunguliwa dhidi ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (Mjibu Maombi).

Waleta Maombi walidai kuwa Mjibu Maombi alikiuka haki zao kuhusiana na uendeshaji wa kesi mbele ya mahakama. Kwa mujibu wa Waleta Maombi, mahakama iliyoendesha kesi ilikosea kwa kuwatia hatiani kwa kuzingatia ushahidi ambao ulikuwa na mashaka na utata ambapo kulikuwa na upotoshwaji; kwamba Mahakama ya Rufaa ilikosea kwa kuzingatia ushahidi wa mashtaka wakati kulikuwa na shaka la msingi ambalo lingeweza kusuluhishwa kwa faida ya Waleta Maombi; kwamba makosa yaliyofanywa na Mahakama ya Rufaa yalikuwa kinyume cha sheria na kusababisha kuharibika kwa haki; na hivyo uamuzi wa mahakama hiyo ulisema ulikiuka haki za msingi za Waleta Maombi na Kifungu cha 3(1) na (2) cha Mkataba.

Kwa upande mwingine, Mjibu Maombi alidai kwamba Mahakama haina mamlaka ya kuhukumu suala hili na aliiomba Mahakama kutupilia mbali Maombi hayo kwa sababu hayajatimiza mahitaji ya ukubalifu yaliyotajwa chini ya Kanuni ya 50(2)(e) (f) ya Kanuni za Mahakama; na kumwamuru Mleta Maombi kubeba gharama.

**MUHTASARI WA HUKUMU**

Mjibu Maombi aliomba kwamba Mahakama ione kwamba hajakiuka Vifungu vya 3(1) na (2) vya Mkataba; kwamba Mahakama inapaswa kutupilia mbali Maombi haya kwa ujumla wake kwa kushindwa kuzingatia sheria; kwamba Mahakama inapaswa kutupilia mbali maombi ya Waleta Maombi; na kuona kwamba gharama za Maombi haya zibebwe na Waleta Maombi.

Kuhusu mamlaka ya kisheria, Mjibu Maombi alidai kwamba Mahakama itakuwa ikifanya kazi kama mahakama ya mwanzo na mahakama ya rufaa kwa kuchunguza masuala yaliyoibuliwa kwa mara ya kwanza au yaliyofungwa na mahakama za ndani hapo awali. Katika suala hili, Mahakama imesisitiza kuwa ina mamlaka ya kusikiliza Maombi chini ya Kifungu cha 3(1) cha Itifaki, kutokana na hiyo inaweza kuchunguza Maombi yoyote yaliyowasilishwa kwake, ilimradi tu haki zinazodaiwa kukiukwa zinalindwa na Mkataba au chombo kingine chochote cha haki za binadamu kilichoidhinishwa na Mjibu Maombi. Mahakama ilisema tena kuwa ingawa haina mamlaka ya mahakama ya rufaa kuhusiana na madai ambayo tayari yamechunguzwa na mahakama za kitaifa, bado ina uwezo wa kutathmini uhalali wa kesi za ndani dhidi ya viwango vilivyowekwa katika vyombo vya kimataifa vya haki za binadamu vilivyoidhinishwa na Serikali husika. Kwa hivyo, Mahakama ilitupilia mbali pingamizi hilo na kubaini kuwa ilikuwa na mamlaka ya kisheria kushughulikia Maombi hayo.

Ingawa hakukuwa na mapingamizi kuhusu mamlaka binafsi, ya muda na ya kieneo ya Mahakama, kwa mujibu wa Kanuni ya 46(1) ya Kanuni za Mahakama, hata hivyo Mahakama ilichunguza vipengele vingine vyote vya mamlaka yake na kubaini kwamba ilikuwa na mamlaka ya kusikiliza Maombi.

Kuhusu ukubalifu wa Maombi, Mahakama, ilizingatia pingamizi lililowekwa na Mjibu Maombi, kuhusiana na ufaafu wa muda baada ya kukakamilisha taratibu za ndani ambapo Maombi yaliwasilishwa. Mahakama ilibaini kuwa wakati ambao Maombi yaliwasilishwa, yaani miaka miwili (2) na mwezi mmoja (1), ni mwafaka kwa maana ya Kifungu cha 56(6) cha Mkataba, kwa kuzingatia mazingira ya kesi, yaani kwamba Waleta Maombi hawana ujuzi wa sheria na kwamba wakati wa kuwasilisha Maombi, walikuwa wamefungwa na kwa hivyo hawakuwa na uhuru wa kufanya mizunguko.

Mahakama ilikuwa imeridhishwa kwamba kumbukumbu ilionyesha kwamba masharti yote ya ukubalifu kama yalivyowekwa kwenye Kifungu cha 56 cha Mkataba na kutamkwa tena katika Kanuni ya 50 (2) ya Kanuni za Mahakama yalikuwa yamezingatiwa; yaani kwamba utambulisho wa Waleta Maombi unajulikana ; Maombi yanazingatia Mkataba wa Umoja wa Afrika na Mkataba; Maombi hayajaandikwa kwa lugha ya kudharau; taratibu za ndani zilikamilika; na Maombi hayaibui masuala ambayo yalisuluhishwa hapo nyuma.

Baada ya kuona kuwa Maombi haya yanakubalika, Mahakama iliangalia endapo Mjibu Maombi alikiuka

haki za Waleta Maombi kama ilivyodaiwa.

Kwanza, Waleta Maombi wanadai kwamba Mjibu Maombi alikiuka haki zao za kuwa na haki sawa mbele ya sheria na ulinzi sawa wa sheria chini ya Kifungu cha 3 cha Mkataba ambapo mahakama za ndani ziliwakuta na hatia na kuwahukumu kulingana na ushahidi ambao haukukidhi viwango vinavyotakiwa.

Kuhusiana na madai ya Waleta Maombi kwamba Mjibu Maombi alikiuka Kifungu cha 3 cha Mkataba kuhusiana na haki ya ulinzi sawa wa sheria, Mahakama ilibainisha kuwa kutokana na kumbukumbu ya Maombi ya sasa, hakuna ushahidi wa athari kwamba kesi za ndani ziliendeshwa kulingana na sheria au amri yoyote, ambayo inajumuisha masharti tofauti kwa Waleta Maombi ikilinganishwa na watu wengine wenye kasi kama ya Waleta Maombi katika masuala ya uthibitisho na ushahidi. Mahakama hii ilibainisha kuwa, kama inavyoonekana kwenye kumbukumbu, Mahakama ya Rufaa ilichunguza ushahidi wote uliowasilishwa na upande wa mashtaka lakini hatimaye ikatupilia mbali ushahidi huo, jambo lililoonekana kuwa linaleta mkanganyiko. Mahakama iliamua kwamba haiwezi kusemwa kuwa haki ya usawa mbele ya sheria ilikiukwa kwa sababu tu kwamba Mahakama ya Rufaa hatimaye ilitupilia mbali ushahidi ulioleta mkanganyiko ambao Waleta Maombi wanadai ungewanufaisha wao. Kwa kuzingatia yaliyotajwa hapo juu, Mahakama ilitupilia mbali madai ya Waleta Maombi kwamba Mjibu Maombi alikiuka Kifungu cha 3 cha Mkataba kuhusu jinsi Mahakama ya Rufaa ilivyoamua masuala ya uthibitisho na ushahidi.

Pili, Waleta Maombi wanadai kuwa uamuzi wa Mahakama ya Rufaa kutupilia mbali rufaa yao, kuweka kando hukumu ya kifungo cha miaka thelathini (30) na badala yake kutoa hukumu ya kifungo cha maisha kuliwaacha wakiwa na uchungu mkubwa na bila fursa yoyote ya kukata rufaa.

Mahakama hii ilibainisha kuwa kwa mujibu wa Kifungu cha 131A (1) na (2) cha Sheria ya Adhabu ya Mjibu Maombi, hukumu ya kifungo cha maisha ni lazima kwa kosa la ubakaji unaohusisha kikundi. Mahakama iliamua kuwa ni kwa kuzingatia kifungu kilichotajwa hapo juu ndipo Mahakama ya Rufaa ilirejesha hukumu ya kifungo cha maisha iliyotolewa awali na Mahakama ya Wilaya. Mahakama iliamua kwamba Waleta Maombi hawakuonyesha kwamba kifungu chochote cha sheria husika kiliwalenga wao binafsi au kwamba Mahakama ya Rufaa iliamua rufaa yao kwa namna tofauti ikilinganishwa na wadai wengine walio katika hali inayofanana. Kwa hivyo, Mahakama ilitupilia mbali madai ya Waleta Maombi na ikaona kuwa Mjibu Maombi hakukiuka haki zao kama zilivyohakikishwa chini ya Kifungu cha 3 cha Mkataba.

Katika kesi hii, kwa kuwa hakuna ukiukaji ulioonekana, Mahakama ilitupilia mbali maombi ya fidia ya Waleta Maombi.

Kila upande uliamriwa kubeba gharama zake mwenyewe.

Kwa mujibu wa Kifungu cha 28(7) cha Itifaki na Kanuni ya 70(1) ya Kanuni za Mahakama, Jaji Ben KIOKO, Jaji Tujilane R. CHIZUMILA na Jaji Dennis ADJEI walitoa Maoni ya Pamoja ya Kupinga.

**Maelezo zaidi**

Maelezo zaidi kuhusu kesi hii, ikiwa ni pamoja na hati kamili ya uamuzi wa Mahakama ya Afrika, inaweza kupatikana kwenye tovuti: https://www.african-court.org/cpmt/details-case/0072016

Kwa maswali mengine yoyote, tafadhali wasiliana na Msajili kwa barua pepe registrar@african-court.org.

*Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu ni mahakama ya bara zima iliyoanzishwa na nchi wanachama wa Umoja wa Afrika ili kuhakikisha haki za binadamu na watu barani Afrika zinalindwa. Mamlaka ya Kisheria ya Mahakama kuhusu kesi na mizozo yote iliyowasilishwa kwake kuhusu tafsiri na utekelezaji wa Mkataba wa Afrika kuhusu Haki za Binadamu na Watu na chombo kingine chochote cha Haki za Binadamu kilichoidhinishwa na Nchi zinazohusika. Kwa maelezo zaidi, tafadhali tembelea tovuti yetu www.african-court.org.*